

MAJARIBIO YA MTHANI DARASA LA SITA

MUHULA WA KWANZA-KISWAHILI-2019

1. Hakikisha umeandika

(i) Jina lako

(ii) Jina la shule yako

MUDA: SAA 1 DAK. 40

Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.

Katika msitu mmoja mkubwa, 1 wanyama wengi, 2 mwao 3 mbogo na buibui. Siku moja msitu huu 4 moto. Wanyama wote walishikwa na 5 wakaanza kukimbia ili 6. Mbogo alipokuwa akikimbia, alikutana na buibui 7 amejawa na hofu nyingi.

"Tafadhali bwana mbogo nichukue juu ya pembe zako ili 8 motoni, nami nitakusaidia siku 9." Watu husema, 10 siku za jua mfae siku za mvua. Wakati huu nuru ya mchana ilikuwa inaanza 11 na mara tu jua 12 tukakizingira kile kichaka 13 yule simba, na wengine wetu 14 kwenda na 15.

- | | | | |
|---------------------|------------------|-----------------|------------------|
| 1. A. kaliishi | B. kuliishi | C. kuliisi | D. kuliichi |
| 2. A. katika | B. miongoni | C. mwongoni | D. baadhi |
| 3. A. akiwa | B. wakiweko | C. wakawa | D. wakiwa |
| 4. A. ulishika | B. uliwaka | C. uliteketea | D. uliungua |
| 5. A. wasiwasi | B. maafa | C. waziwazi | D. giza |
| 6. A. watoroke | B. wajiokoe | C. wanufaike | D. wahangaika |
| 7. A. aliyekuwa | B. aliekuwa | C. alikuwa | D. waliyekuwa |
| 8. A. nisijeruhiwe | B. nisichomeke | C. nisiumie | D. nisitekete |
| 9. A. nyingine | B. mwingine | C. ingine | D. mengine |
| 10. A. akuvae | B. akufaae | C. akufaye | D. akufaaye |
| 11. A. kutoka | B. kutokeza | C. kutokosa | D. kutokosha |
| 12. A. ulipochozoza | B. lilipochomoka | C. ulichomoza | D. lilipochozoza |
| 13. A. alipoingia | B. alikoingia | C. aliingia | D. alimoingia |
| 14. A. wakajitolea | B. akajitolea | C. wakijitolea | D. akijitolea |
| 15. A. kumbuburusha | B. kububurusha | C. kubumburusha | D. kumbumburusha |

Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu swali

ukifuata maagizo uliyopewa.

16. Tegua kitendawili:-

Akiondoka hatuonani.

- | | |
|----------|-------------|
| A. Taa | B. Mwangaza |
| C. Tochi | D. Moto |

17. Kanusha:-

Mama ameenda sokoni.

- | |
|--------------------------|
| A. Baba hajaenda sokoni. |
| B. Baba ameenda sokoni. |
| C. Mama hajaenda sokoni. |
| D. Mama hayuko sokoni. |

Darasa la 6 Kisw.

18. Majira ya baridi kali huitwa, e?
A. Masika B. Vuli
C. Kipupwe D. Kiangazi
19. Kamilisha methali:-
Fimbo ya karibu ndiyo _____.
A. haiui nyoka B. haiwau nyoka
C. iuayo nyoka D. huuwa nyoka
20. Konokono husambaza maradhi yaitwayo ____.
A. malaria B. waba
C. kichocho D. malale
21. Kamilisha sentensi:-
Wanafunzi _____ walikosa shule jana.
A. wasita B. watisa
C. wakumi D. sita
22. Mtoto wa nzi ni buu, mtoto wa bata huitwa ____.
A. kifaranga B. kiluwiluwi
C. maige D. kiyoyo
23. Kamilisha tanakali hii:-
Mtambo ulisaga unga _____.
A. demdem B. zii
C. raruru D. tikitiki
24. Ni vazi lipi ambalo huvaliwa na wanawake pekee?
A. Chupi B. Kanchiri
C. Bulibuli D. Surupwenye
25. Nahau kukanyaga chechele humaanisha _____.
A. kuona afueni B. kupotea njia
C. kulima mchele D. kufa kwa kukanyagwa
26. Ni neno lipi ambalo ni kisawe cha mwandani?
A. Hasimu B. Sahibu
C. Hasidi D. Shaibu
27. Maneno ng'ambo, ng'oa, ng'ong'o na yana sauti ya vingo'ong'o. Alama itumiwayo huitwa ya _____.
A. kituo B. kipumuo
C. koma D. ritifaa
28. Mwalimu **mgeni** atajiunga nasi **mwakani**. Maneno yaliyopigiwa kistari ni _____.
A. kitenzi, kivumishi B. kivumishi, kielezi
C. kielezi, kiarifa D. kivumishi, kikusishi
29. Ukigawa mraba mara mbili utapata maumbo ya _____.
A. duara dufu B. miraba miwili
C. mstatili D. nusu kipenyo
30. Anayefunza katika chuo kikuu huitwaje?
A. Shahada B. Mkufuzaji
C. Mhutubu D. Mhadhiri

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.

Moto huweza kuanzishwa kwa njia nyingi. Wakati mwingi huchukuliwa na binadamu kama rafiki, huwakishwa ili kusaidia kuviivisha vyakula kwa njia mbalimbali. Moto **hukokwa** wakati mwingine ili kuwapa watu joto wakati wa baridi.

Kwa upande mwingine, moto huweza kutokea kama ajali na kuua, kuteketeza vitu vya gharama kubwa, majumba, misitu na kuyaharibu mazingira. Kwenye majumba, moto huweza kuanzishwa na hitilafu na umeme au gesi, stovu na matumizi mabaya ya mafiuta ya taa, petroli au makaa.

Iwapo moto utatokea popote, jaribu kuuzima mara moja. Ukiona kuwa umezidi, piga kelele kuomba msaada kuuzima huku ukijiepusha na hatari kama kuna simu wapigie wazima moto wafike mahali hapo haraka.

Kama kuna vifaa vya kuzimia moto, vitumie. Jaribu kuondoa vitu ambavyo ni muhimu na hasa vile vinavyoweza kueneza moto. Zima sehemu zote zinazoweza kuwa chanzo cha moto. Madirisha na milango ya sehemu zilizofungwa zifunguliwe bila hofu. Ukiona moto umezidi, toka nje kwa haraka huku ukiwaamrisha wengine walioimo ndani kutoka nje pia.

- | | |
|---|--|
| <p>31. Njia gani isiyo ya manufaa kati ya zile ulizopewa kuhusu moto?</p> <p>A. Kufukuza wanyama mwituni</p> <p>B. Kuivisha vyakula</p> <p>C. Kuwapa watu joto</p> <p>D. Kuchoma nyama</p> <p>32. Iwapo moto utatokea popote _____</p> <p>A. ingia nyumbani na ukae kitako</p> <p>B. jifunike kwa matawi</p> <p>C. piga kamsa kwa ajili ya usaidizi</p> <p>D. nyunyizia petroli</p> <p>33. Ni njia zipi ambazo moto hauanzishwi majumbani?</p> <p>A. Hitilafu za umeme</p> <p>B. Gesi na stovu</p> <p>C. Petroli au makaa</p> <p>D. Uvutaji wa sigara</p> <p>34. Moto ukizidi, ni hatua gani huchukuliwa?</p> <p>A. Kufunga madirisha</p> <p>B. Kufungua milango</p> <p>C. Kunyunyizia maji</p> <p>D. Waite wazima moto</p> | <p>35. Vitu vipi vinavyoweza kueneza moto?</p> <p>A. Madirisha B. Milango</p> <p>C. Petroli D. Mabati</p> <p>36. Moto hukokwa maana yake ni _____</p> <p>A. huzimwa B. hutayarishwa</p> <p>C. huenezwa D. huababishwa</p> <p>37. Njia ipi ambayo chakula hakiivishwi?</p> <p>A. Hukaangwa B. Huchomwa</p> <p>C. Huhifadhiwa D. Huchemshwa</p> <p>38. Kwa nini moto ni rafiki kwa binadamu?</p> <p>A. Huteketeza misitu</p> <p>B. Huhifadhi wanyamapori</p> <p>C. Huwapasha joto watu nyakati za kipupwe</p> <p>D. Hukokwa wakati watu wanahisi njaa</p> <p>39. Jina majumba ni wingi wa nomino ipi?</p> <p>A. Nyumba B. Chumba</p> <p>C. Jumba D. Kijumba</p> <p>40. Kichwa kinachostahili ufahamu huu ni _____</p> <p>A. Kuzimwa kwa moto</p> <p>B. Usaidizi wa moto</p> <p>C. Mikasa ya moto</p> <p>D. Kukokwa kwa moto</p> |
|---|--|

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.

Hivi majuzi mwituni kulikuwa na mkutano wa wazee wa porini. Huko, tembo aliwaambia wanyama wakubwa kuwa alikuwa ameifanyia utafiti tabia ya fisi. Alionekana **kughasika** mno. Aliamua kushauriana na wanyama wakubwa ili wamuonye fisi na kumshawishi kuuacha ulafi.

Wakamwita fisi, jambo lililowashangaza wanyama hao waheshimiwa ni kuwa fisi hakukataa mwito wala hawakuwakata karima. Alimkodolea tu macho kila aliyekuwa akisema, huku akimbeua. Baada ya kupata michapo yote na nasaha zote, hapo alianza kujishaua kwa madaha ya ujana.

Darasa la 6 Kisw.

"Wazee wangu ninawashukuru kwa hayo yote, lakini mazoea yana shida. Nyinyi nanyi mna ubaradhuli. Hata mfanye nini daima dawamu, nitaionea fahari tabia hiyo yangu."

- | | |
|---|--|
| <p>41. Kulingana na hadithi hii, fisi alitwa na wanyama kwa nini?</p> <p>A. Atoe macho</p> <p>B. Ashawishiwe aache ulafi</p> <p>C. Aonywe asile kwa pupa</p> <p>D. Afanyiwe utafiti</p> <p>42. Mwituni kulikuwa na nini?</p> <p>A. Wazee wa porini</p> <p>B. Fisi na simba</p> <p>C. Kikao cha wazee</p> <p>D. Mkutano wa wazee wa porini</p> <p>43. Ni sahihi kusema _____.</p> <p>A. fisi alikaribisha nasaha ya wazee kwa furaha</p> <p>B. fisi aliacha ulafi</p> <p>C. fisi hakukataa mwito</p> <p>D. fisi aliukataa mwito</p> <p>44. "..... <i>alionekana kughasika sana</i>....."</p> <p>Maana yake ni?</p> <p>A. Kufurahia</p> <p>B. Kusikika</p> <p>C. Kukereka</p> <p>D. Kusikika</p> <p>45. Nani aliyekuwa ameifanyia utafiti sana tabia ya fisi?</p> <p>A. Ndovu</p> <p>B. Sungura</p> <p>C. Wanyama</p> <p>D. Simba</p> | <p>46. Nani walikuwa wenye ubadhirifu?</p> <p>A. Walafii</p> <p>B. Vijana</p> <p>C. Ndovu</p> <p>D. Wanyama</p> <p>47. Fisi aliwashukuru wazee kwa sababu _____.</p> <p>A. walimshauri visivyo</p> <p>B. nasaha yao ilikuwa ya ungwana</p> <p>C. kwa fisi ilikuwa ni kejeli tu</p> <p>D. walimpongeza kwa usikivu wake</p> <p>48. Mimi kawaida hupenda kuchangamkia maakuli. Maana yake ni _____.</p> <p>A. hupenda kupapia mlo</p> <p>B. hupenda kufurahikia mlo</p> <p>C. hupenda kula kistarehe</p> <p>D. hupenda masazo ya chakula</p> <p>49. "<i>Akimbeua</i>," maana yake ni _____.</p> <p>A. akikereka</p> <p>B. akiiba</p> <p>C. akiudhika</p> <p>D. akimdharau</p> <p>50. Kichwa kifaacho kwa hadithi hii ni nini?</p> <p>A. Kikao cha wazee</p> <p>B. Tamaa ya fisi</p> <p>C. Ushauri nasaha</p> <p>D. Madaha ya ujana</p> |
|---|--|